**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO**

**SIMU:**
Mkuu wa Shule:
**0757841015/0676841015**
Makamu Mkuu wa Shule:
**0765504646/0714925245**.
…………………………..
kasandasecondaryschool@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI KASANDA
S.L.P 03,
**KAKONKO,**

TAREHE

---

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.**

..........................................…………………….………………………………...

S.L.P ……………………………………………………….……………………….

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASANDA HALMASHAURI YA KAKONKO MKOA WA KIGOMA MWAKA ………………**

TAHASUSI…………………………………….............………..................…..

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Kasanda kwa mwaka ………… na atasoma tahasusi ya**; (PCB, CBG)**

Shule ya Sekondari Kasanda ipo umbali wa Kilometa 4 kutoka kituo Cha mabasi Cha Mji wa kasanda, kata ya Kasanda nauli shilingi 3000 tu Hadi shuleni. Ukitokea wilaya ya Biharamulo Kasanda iko mbele ya stendi kuu ya mabasi Kakonko mjini na ukitokea wilaya ya Kibondo Kasanda ipo kabla ya kituo Cha mabasi Kakanko mjini

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

### 2.1 Sare za Shule

2.1.1 Wasichana

a) Sketi mbili rangi ya kijivu nyeusi (dark grey kitambaa "ISTEM NA:2") yenye urefu hadi kwenye kifundo cha mguu na yenye mshono wa marinda box ( rinda Kubwa mbele na nyuma na marinda matatu upande wa kulia na kushoto), hii ni Sare ya darasani Sketi hizo pia unaweza kuzipata shuleni kwa TSH 20,000/- kila moja.
b) Nguo za kushindia (shamba dress) ni sketi mbili za rangi ya blue bahari (kitambaa cha "ISTEM NO:2") ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu, mshono wa marinda box kama ilivyo sketi ya darasani, vile vile unaweza kuipata shuleni kwa TSH 20,000/- kila moja.
c) Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisizobana zenye vifungo vya kawaida.
d) Tai ndefu rangi ya damu ya mzee, unaweza pia ukaipata shuleni kwa shilingi 4000 tu.
e) Soksi nyeupe jozi mbili.
f) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye Kamba, na visigino vifupi. (Bajaji na yeboyebo haziruhusiwi kabisa).
g) T-shirt za shule mbili zenye Nembo ya Shule utazipata shuleni kwa gharama ya shilingi 10000/= kila moja.
h) kwa waislamu wataruhusiwa kuvaa Hijabu nyeupe darasani na Hijabu ya rangi ya Zambarau (purple) kama vazi la kushindia, ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
i) Sweta la rangi ya kijivu vyeusi lenye nembo ya shule utalipata shuleni kwa shilingi 15000/=
j) Aje na ndala za kuogea na viatu vya kushindia. (SIMPLE ISIYO NA MAUA JUU MOSIMO SHOES, SANDLES ZA NGOZI ZENYE MIKANDA NYUMA YA KISIGINO)
k) mwanafunzi anatakiwa kunyoa nywele kawaida **sio kiduku**
l) Full tracksuit kwa mwanafunzi rangi ya kijivu nyeusi yenye mchirizi mweupe.( Ataripoti shuleni akiwa amevaa).

2.1.2 Wavulana:

a) Suruali mbili za kijivu nyeusi (dark grey) za darasani zenye mifuko mitatu na tai ndefu ya rangi ya damu ya mzee. Na suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana sio chini ya inch 17. (**SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI**). (Suruali hizo unaweza kuzipata shuleni pia kwa shilingi 18,000/- Kwa kila moja)

b) Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisibane zenye vifungo vya kawaida.

c) Soksi nyeusi jozi mbili.

d) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali mbili za rangi ya blue bahari zenye mifuko mitatu. Na suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana wa chini zisipungue inch 17 (unaweza pia kuzipata shuleni kwa shilingi 18,000/- Kila moja). **(SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI).**

e) T-shirt za shule mbili zenye Nembo ya Shule. (zinapatikana shuleni tu kwa shilingi 10,000/- Kwa kila moja.)

f) Sweta la rangi ya kijani jeshi (unaweza pia kulipata shuleni kwa shilingi 15000/-).

g) Tai ndefu ya damu ya mzee, unaweza pia ukaipata shuleni kwa shilingi 4000 tu.

h) Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye Kamba, na visigino vifupi. (Bajaji na yeboyebo haziruhusiwi kabisa).

i) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

j) j) Aje na ndala za kuogea na viatu vya kushindia.(raba, sandles zenye mikanda)

k) full tracksuit kwa mwanafunzi rangi ya bluu-bahari yenye mchirizi mweupe. (ataripoti akiwa amevaa) NB.

- **Nguo nyingine zozote mbali na sare zilizotajwa hapo juu haziruhusiwi. (Mwanafunzi ataripoti shuleni akiwa amevaa truck sut.)**
- **Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi (kunyoa) wakati wote wawapo shuleni.**

2.1.3 Sare za Michezo

a) Raba za michezo kwa wanafunzi wote
b) Bukta na t-shirt za rangi ya bluu yenye michirizi mieupe kwa wavulana na wasichana.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Daftari 10 (counter books)
ii. Ream 2 za Karatasi (A4) kwa mwaka aina ya double A
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika aliyochaguliwa mwanafunzi
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator zinapatikana pia eneo la jirani na shule 45,000/=
vi. Godoro linapatikana shuleni kwa kukodi kwa mwaka shilingi 25000/= hivyo mwanafunzi asije na godoro maana halitapokelewa kabisa.
vii. Mashuka Jozi 2 (rangi ya pink 1 na blue 1), blanket 1, foronya ya godoro (bed cover) ya rangi ya dark blue1, chandarua 1 cha rangi ya blue.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. kwa wanafunzi wote PCB &CBG aje na vifaa vya usafi vifuatavyo: Kwanja 1, jembe 1, shoka 1, mifagio 2 (hard bloom na soft bloom), ndoo 2 lita kumi na Squeezer -1
xi. Sanduku la chuma la kutunzia vitu vyake( trunker)

**NB; Mwanafunzi aje na bima ya afya ili imsaidie katika gharama za matibabu kwa kipindi awapo shuleni.**

**2.3 Michango mbalimbali**

| No. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji | 65000 |
| 2 | tahadhari | 5000 |
| 3 | nembo | 5000 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5000 |
| | jumla | 80000 |

- Michango hiyo ilipwe kwenye akaunti **No: 51501100049-NMB** jina la akaunti

**KASANDA SEC. SCHOOL-REVENUE COLLECT,** aje na risiti ya malipo ya benki afikapo shule.

## 1. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WM– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Mwanafunzi atatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na alfajili( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule ikiwa atapata changamoto kama vile Msiba au Ugonjwa.

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. kusuka nywele na kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni; xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule bila kufuata utaratibu uliowekwe.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, kujinyonga, NK na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.


**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu; na
v. Kivuli cha matokeo ya kidato cha IV (result slip).

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA KASANDA KWA TAALUMA BORA**



…………………………………..
**JAPHET TUYATE SAFARI** MKUU
WA SHULE.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KASANDA
S.L.P 03 KAKONKO

## HISTORIA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la mwanafunzi
..........................................................................................................

2. Jina la baba
..........................................................................................................

3. Jina la mama.
..........................................................................................................

4. Jina kamili la mlezi.
........................................................................................................

5. Anuani ya mzazi/mlezi.
..........................................................................................................

6. Uhusiano wa mlezi.
..........................................................................................................

7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) 8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni:
..........................................................................................................

9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni:
..........................................................................................................

10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni.
..........................................................................................................

11. Afya ya mwanafunzi, Kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

12. Madhehebu ya dini
..........................................................................................................

13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

1. …………………………………………………………………………………...............
2. …………………………………………………………………………………...............
3. …………………………………………………………………………………...............
4. …………………………………………………………………………………...............

## KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.

Jina la mwanafunzi.

.........................................................................................................................

Jina la mzazi/mlezi.

.........................................................................................................................

Anuani ya mzazi/mlezi.

.........................................................................................................................

Uhusiano ……………………………………...(mjomba, shangazi, kaka, dada).

Mimi ………........................................................................nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.

Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni,nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi …………………………..........................................................

Tarehe...........................................................................................................................

Mimi ………………………………………………..............……………… mzazi/mlezi wa mwanafunzi.

………………………………………………………………..........................................

ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi……………………………….........................................................

Tarehe......……………….........................................………………………….................

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

Student'S name.

………………………………………………………………………………

Age.

………………………………………………………………………………

Stool Test

………………………………………………………………………………

Blood group.

………………………………………………………………………………

Urine analysis

………………………………………………………………………………

Sphills test

………………………………………………………………………………

Chest test.

………………………………………………………………………………

Speech

………………………………………………………………………………

Eye test.

………………………………………………………………………………

Abdomen.

………………………………………………………………………………

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education.

………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

Signed.

………………………………………………………………………………

Designation.

………………………………………………………………………………

Official stamp.

………………………………………………………………………………

Date.

………………………………………………………………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI).**

**SHULE YA SEKONDARI KASANDA.**

**AHADI YA MZAZI:**

---

Mimi……………………………………………………………………………………

(Jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa

……………………………………………………………………………………

kidato cha……………………………………………………………………………

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema.Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia mwanangu malezi na elimu bora kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.Na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapo takiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi

……………………………………………………………………………………

Anuani kamili

……………………………………………………………………………………

Simu

……………………………………………………………………………………

Tarehe

……………………………………………………………………………………